# KATIBA YA JUMUIYA YA WATENGENEZAJI WA VYAKULA VYA MIFUGO TANZANIA ( TAFMA ).

IMEKUBALIWA NA WANACHAMA
TAREHE 30 MWEZI WA KWANZA, 1990

DAR ES SALAAM.

YALIYOMO

IBARA YA KATIBA


| | ukurasa |
|---|---|
| 1.Dibaji | 3 |
| 2. Jina la Jumuiya | 3 |
| 3. Malengo Makuu | 3 - 4 |
| 4. Uanachama | 4 |
| 5. Chombo Kikuu na Maofisa (Kamati ya Utendaji) | 4 - 5 |
| 6.Uchaguzi na Muda wa Kudumu Madarakani | 5 - 6 |
| 7. Wajibu wa kamati ya Utendaji | 6 |
| 8. Uwezo wa Kutunga Sheria | 6 |
| 9. Muhuri wa Pamoja | 6 |
| 10. Uwezo wa Kurekebisha Katiba | 6 |
| 11. Kuvunjwa kwa Jumuiya | 7 |
| 12. Fidia | 7 |
| 13. Sheria Ndogo | 7 - 13 |

**KATIBA YA JUMUIYA YA WATENGENEZAJI WA VYAKULA VYA MIFUGO TANZANIA ( TAFMA ).**

**Ibara ya 1. Dibaji.**

Kwamba wengi wa watengenezaji wa vyakula vya mifugo Tanzania waliopo nchini Tanzania wameonyesha nia yao ya kuunda Jumuiya, Katiba hii, inashuhudia kuundwa kwa Jumuiya hiyo kama inavyooneka hapa chini.

**IBARA YA 2. JINA LA JUMUIYA**

Jumuiya itaitwa Jumuiya ya watengenezaji wa Chakula cha Mifugo Tanzania.

Katika muktadha ufuatao, ambapo neno Jumuiya linaonekana inatakiwa kueleweka kwa maana ya Jumuiya ya Watengenezaji wa Chakula cha Mifugo Tanzania.

**IBARA YA 3. MALENGO MAKUU.**

3.1. Kutoa baraza moja kwa watengenezaji wote wa chakula cha mifugo Tanzania.

3.2. Kuwa kiungo cha kushirikiana na chombo cha Serikali juu ya mambo yote yanayohusiana na utengenezaji wa chakula cha mifugo ndani ya nchi. kwa mfano:-
(a) Utoaji wa malighafi kadhaa.
(b) Uuzaji wa bidhaa za Jumuiya.

3.3. Kuwa kiungo baina ya Jumuiya na wafugaji.

3.4. Kuhakikisha kuwa bidhaa zote za wanachama wa Jumuiya hatua kwa hatua zinakidhi viwango vinavyokubalika.

3.5. Kuingia makubaliano yoyote na mashirika, Makampuni au watu wowote ambao wanaweza kuonekana wenye kufaa ili

kufikia malengo ya jumuiya au yoyote kati yao na kupata kutoka shirika, Kampuni au mtu yoyote kati yao, mikataba, sheria, haki, fursa, makubaliano ambayo jumuiya inaweza kudhani inafaa, na kutimiza, kutekeleza na kushikamana na mikataba, sheria, haki, fursa na makubaliano.

3.6. Kufanya kazi kama mdhamini wa wanachama wake wakati wowote ikitokea mahitaji hasa katika upatikanaji wa viambata vya lazima kwa ajili ya utengenezaji wa chakula cha mifugo.

3.7. Kushauri, Kutaarifu au kuongoza wanachama juu ya hatua mpya katika sekta ya chakula cha mifugo ili kuwaweka sambamba na mabadiliko yanayojitokeza katika nchi nyingine.

**IBARA YA 4. UANACHAMA.**

4.1. Uanachama utakuwa wazi kwa watengenezaji wote wa vyakula vya mifugo kwa ajili ya biashara.

4.2. Taasisi nyingine yoyote inayojihusisha na maendeleo ya mifugo kama itakavyo kubaliwa na Jumuiya.

Uwanachama utakubaliwa katika mkutano wa kamati ya utendaji na taarifa kutolewa kwa Mkutano Mkuu wa Mwaka.

**IBARA YA 5. CHOMBO KIKUU NA MAOFISA.**

5.1. Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ambayo itaundwa na wafuataao:-

(a) Maafisa wakuchaguliwa:-
Mwenyekiti
Makamu Mwenyekiti
Katibu
Mweka Hazina
Wajumbe wawili wa kamati

(b) Maofisa Wastaafu wa TAFMA.
Maafisa Wastaafu wawili wasiopigiwa kura watakaoteuliwa na maafisa wa kamati ya utendaji wa kuchaguliwa.

Kamati ya utendaji itachaguliwa kulingana na ibara ya 6 ya katiba hii.

5.2. Uendeshaji wa mambo na shughuli za Jumuiya itakuwa dhamana ya Kamati ya Utendaji ambayo itakuwa na uwezo wote juu ya mambo hayo na itafanya kazi zote na mambo yote yahusuyo dhamana hiyo kama ambavyo zingefanywa na Jumuiya na ambazo kwa hapa na kulingana na sheria ndogo hazitakiwi kufanywa na Jumuiya. Katika Mkutano Mkuu lakini hapana ongezeko, punguzo au badiliko la sheria ndogo litakalobatilisha kitendo chochote kilichopita cha Kamati ya Utendaji ambacho kisingetakiwa kufanywa.

**IBARA YA 6. UCHAGUZI NA MUDA WA KUDUMU MADARAKANI KWA KAMATI YA UTENDAJI.**

6.1. Kamati ya Utendaji itachaguliwa na wanachama kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka.

**6.2. STAHIKI YA KUSHIRIKI UCHAGUZI.**

(a) Mwanachama yoyote anaweza kuchaguliwa kushiriki kwenye Kamati ya Utendaji alimradi kuna pendekezo na uungwaji mkono kwa maandishi au kwa kauli ya mdomo na mpendekezwaji lazima aoneshe utayari wake, nia ya kusimama kama mgombea kwenye uchaguzi.

(b) Mpendekezwaji lazima awe mwanachama hai wa kiwanda cha kutengeneza vyakula vya mifugo ki biashara.

**6.3. MUDA WA KUDUMU MADARAKANI.**

Muda wa kudumu madarakani kwa Kamati yote ya Utendaji itakuwa ni miaka mitatu (3).

6.4. Wanachama waliomaliza muda wao wa kubaki ofisini/ madarakani ½ ya wanakamati wanaweza kugombea tena nafasi.

6.5. KUJAZWA KWA NAFASI ISIYO YA KUDUMU.

Kamati ya Utendaji itakuwa na uwezo wa kujaza nafasi wazi ya dharura ili kukamilisha muda wa madaraka ulioachwa wazi na yoyote miongoni mwa wajumbe wote wa kamati. Jambo hili linalazimika kufanyika ndani ya siku 45 baada ya nafasi husika kuwa wazi

**IBARA YA 7. WAJIBU WA KAMATI YA UTENDAJI.**

Kuendesha shughuli za kila siku za Jumuiya na kuhakikisha kuwa malengo ya Jumuiya yanafikiwa kulingana na madaraka iliyopewa na ibara ya 5 na ibara ya 13.

**IBARA YA 8. UWEZO WA KUTUNGA SHERIA NDOGO.**

Kwa azimio lililopitishwa na si chini ya theluthi mbili ya wajumbe waliopo na wanaopiga kura kwenye Mkutano Mkuu, jumuiya inaweza kutoka wakati mmoja hadi mwingine kutunga sheria ndogo kwa ajili ya kurekebisha mambo ya jumuiya kadri itakavyoona inafaa na kutoka wakati mmoja hadi mwingine inaweza kubatilisha au kubadilisha sheria ndogo hizo kwa mbadala alimradi sheria ndogo hizo kwa namna yoyote ile hazipingani na vifungu vya katiba ya jumuiya.

**IBARA YA 9. MUHURI WA PAMOJA.**

Kutakuwa na muhuri mmoja wa Jumuiya ambao utawekwa kwenye mikataba yote na mambo yote yanayohitaji Muhuri wa Jumuiya.

Mambo hayo yanayohitaji muhuri wa Jumuiya yatakuwa yanakubaliwa kwenye mkutano wa Kamati ya Utendaji na kuwekwa kwa muhuri kuwe kumeshuhudiwa na wajumbe wowote wawili wa Kamati ya Utendaji.

**IBARA YA 10. UWEZO WA KUREKEBISHA KATIBA.**

Kutakuwa na azimio lililopitishwa na si chini ya theluthi mbili ya wajumbe waliopo na waliopiga kura (wenyewe binafsi au kwa wawakilishi) kwenye Mkutano Mkuu ulioitishwa kulingana na

sheria ndogo za Jumuiya. Jumuiya inaweza kutoka wakati mmoja hadi mwingine kubadilisha, kurekebisha au kuongeza kifungu kwenye katiba hii.

**IBARA YA 11. KUVUNJIKA KWA JUMUIYA.**

11.1. Jumuiya inaweza kuvunjwa kwa azimio lililopitishwa kwa ajili ya jambo hilo na theluthi mbili ya kura za wajumbe wote waliosajiliwa kwenye mkutano mkuu usio wa kawaida ulioitishwa mahsusi kwa lengo hilo.

11.2. Kulingana na ibara ya 11.1. hapo juu, mkutano mkuu utateuwa mtu au watu ili awe/wawe mufilisi / wafilisi na kutengeneza vifungu kwa ajili ya kugawanywa kwa rasilimali za Jumuiya.

**IBARA YA 12. FIDIA.**

Kulingana na vifungu vya katiba hii, mwanachama yoyote aliyeajiriwa na Jumuiya katika kamati ya utendaji atafidiwa kutoka kwenye rasilimali za Jumuiya dhidi ya gharama, tozo, hasara na dhima zozote ambazo anaweza kuzipata akiwa katika utekelezaji wa shughuli zake za kiofisi au zinazohusiana na hilo, alimradi vitendo vyake vilikuwa vya msingi na vyenye kuzingatia hali zote kwa busara , ujuzi na weledi.

**IBARA YA 13. SHERIA NDOGO**

Sheria Ndogo No. 1 – Tafsiri.

Sheria ndogo hizi zitaanza kutumika rasmi tarehe……..1990 zikiwa zimepitishwa na theluthi mbili ya wanachama kulingana na ibara ya 8 ya katiba. Katika sheria ndogo hizi, bila ya kuathiri mazingira.

1.1. "Jumuiya" Inamaanisha Jumuiya ya Watengenezaji wa vyakula vya mifugo Tanzania.

1.2. Kamati ya Utendaji – Inamaanisha Kamati halali iliyo madarakani , kwa ajili ya kuendesha mambo ya Jumuiya.

1.3. Wanachama – Inamaanisha, Wanachama wa Jumuiya kama ilivyotajwa chini ya ibara ya 4 ya katiba.

**SHERIA NDOGO NO. 2. WANACHAMA.**

2.1. Kukubaliwa uwanachama kwa watu wote kutafanywa na kamati ya utendaji. Kamati inaweza kwa kutumia busara yake kamili, kwa azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Kamati ya Utendaji kumkatalia uwanachama wa Jumuiya mtu yoyote ambaye itamuona kutofaa kupewa uwanachama. Kamati haitolazimika kutoa sababu zilizopelekea maamuzi yake.

2.2. Hapana ombi lolote la kukubaliwa uanachama litakalozingatiwa na Kamati ya Utendaji bila ya muombaji kukubali kulipa kwa Jumuiya kiwango cha ada ya kujiung a uwanachama kitakachoambatana na ada ya michango ya mwaka anachotakiwa kulipa kwa mwaka anaoomba kujiunga na Jumuiya, ada ya kujiunga uwanachama na ada ya michango ya mwaka zitaamuliwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya baada ya mapendekezo ya Kamati ya utendaji.

2.3. Mwanachama yeyote atakayeshindwa kulipa ada ya michango ya mwaka anayotakiwa kulipa mpaka tarehe 31 mwezi wa 12 katika mwaka ambao kiwango hicho kinapaswa kulipwa na mwanachama yoyote, atakayeshindwa kulipa kiwango kilichoongezeka cha ada ya michango ya mwaka anachotakiwa kulipa kabla ya kumalizika kwa muda wa miezi mitatu baada ya ongezeko kupaswa kulipwa atapoteza sifa za uwanachama, labda endapo Kamati ya Utendaji itaamua vinginevyo juu ya jambo hili au katika shughuli zake za kiutendaji.

2.4. Endapo mwanachama ataamuliwa kuwa muflisi atasimama mara moja kuwa mwanachama.

## SHERIA NDOGO NO. 3. MIKUTANO YA KAMATI YA UTENDAJI.

3.1. Kamati ya Utendaji inalazimika kukutana angalau kila miezi mitatu au zaidi itakapobidi.

3.2. Akidi katika Mkutano wa Kamati ya Utendaji ni wajumbe watatu.

3.3. Mwenyekiti au ikitokea Mwenyekiti kutokuwepo, Makamu Mwenyekiti atachukua kiti cha Mikutano ya Kamati ya Utendaji au ikitokea katika mkutano wowote, wote wawili kutokuwepo, wajumbe waliopo watamchagua mmoja kati yao kuwa Mwenyekiti.

3.4. Mjumbe wa Kamati ya Utendaji analazimika kuhudhuria angalau mikutano mitatu katika wakati wake wa kudumu madarakani. Atahesabiwa kuwa amejiuzulu ikiwa hakutoa sababu za msingi.

3.5. Kamati ya Utendaji itakuwa ndio chombo chenye uwezo na wajibu wa kuwajibisha.

3.6. Ikitokea Kamati kushindwa kumuwajibisha mjumbe yeyote wa Kamati au mjumbe yoyote wa kawaida, muathiriwa yoyote au mtu yoyote aliyeathiriwa na hali hiyo, anaweza kuwasilisha shauri kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka.

## SHERIA NDOGO NO. 4. KAMATI NYINGINE.

4.1. Kamati ya Utendaji inaweza kutoka wakati mmoja hadi mwingine kuanzisha kamati nyingine au kamati ndogo ndogo kwa ajili ya uendeshaji fanisi wa mambo ya Jumuiya.

4.2. Kamati ya Utendaji itateuwa Mwenyekiti wa kila Kamati kutoka miongoni mwa wajumbe na idadi ya wajumbe wa kila Kamati kutoka miongoni mwao au kutoka nje ya Kamati Tendaji na vile vile itaamua muda wa kudumu madarakani na hadidu za rejea.

4.3. Kamati ya Utendaji inaweza kwa kutumia busara yake ya hali ya juu, kuongeza idadi ya wajumbe wa Kamati .

4.4. Kwenye Mkutano wowote wa Kamati au Kamati Ndogo akidi ni 50% ya wajumbe.

**SHERIA NDOGO NO. 5. MIKUTANO.**

5.1. Mkutano Mkuu wa Mwaka utaitishwa si zaidi ya miezi 6 baada ya mwaka wa fedha kukamilika na utajadili mambo yafuatayo:-

(a) Kupokea taarifa ya mwaka ya Kamati ya Utendaji

(b) Kupokea mahesabu yaliyohakikiwa ya mwaka uliopita

(c) Kuzingatia na kupokea wanachama wapya wa Jumuiya

(d) Kuchagua wajumbe wa Kamati ya Utendaji watakaochukua nafasi za wale waliomaliza muda.

(e) Kuteua na kupanga mishahara ya Mkaguzi wa mahesabu kwa mwaka mpya.

(f) Kufanya shughuli zingine zozote.

5.2. Mwanachama anayetaka kuleta mbele ya Mkutano Mkuu wa Mwaka hoja yeyote isiyohusiana na mambo ya kawaida ya mwaka yahusuyo Jumuiya anaweza kufanya hivyo kwa sharti:-

(a) Kwamba taarifa kwa maandishi ya hoja iliyopendekezwa itumwe au apewe Katibu na ipokelewe naye si zaidi ya siku 45 kabla ya tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.

(b) Kwamba taarifa ya hoja iliyopendekezwa iambatane na taarifa za maandishi kutoka, kwa si chini ya wajumbe wawili wenye haki ya kupiga kura kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wakionesha matakwa yao kwamba hoja

iliyopendekezwa iletwe mbele ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.

(c) Kwamba hoja iliyopendekezwa inahusiana na mambo ya Jumuiya.

5.3. Mkutano Mkuu usio wa kawaida unaweza kuitishwa kulingana na azimio la Kamati ya Utendaji au kwa ombi la Mwenyekiti au kutokana na (matakwa) mahitaji yaliyosainiwa na wanachama theluthi moja ( 1/3 ) au zaidi wa Jumuiya.

Kwa matakwa hayo, kufanyiwa kazi ni lazima yaambatane na arbuni (deposit) ya pesa ambayo kwa maoni ya kamati ya utendaji zinatosha kukabili gharama zinazohusiana na kuwaita wajumbe na kuitisha mkutano.

Katibu ataitisha Mkutano Mkuu wa Dharura akieleza kikamilifu malengo ya kuitisha Mkutano huo. Mkutano Mkuu wowote kama huo utaitishwa ndani ya siku ishirini na nane (28) za kupitisha azimio hilo au kupokea ombi hilo au matakwa ya kufanya hivyo.

Endapo pendekezo la matakwa litakubaliwa arbuni (deposit) itarudishwa kikamilifu.

5.4. Mkutano Mkuu wa Mwaka au Mkutano Mkuu wa Dharura utaitishwa kwa taarifa ya maandishi ya angalau siku 14. Taarifa haitozingatia siku ambayo imetumwa au ingetakiwa kutumwa na siku iliyotolewa na itaonesha pahala, siku na saa ya Mkutano na kuhusu suala la jambo lisilo shughuli ya kawaida ya mwaka ihusuyo Jumuiya, taarifa itaonesha asili ya uhusiano wa jambo hilo. Kuhusu Mkutano Mkuu wa Mwaka Katibu atatuma kwa kila mjumbe kivuli cha taarifa ya mwaka ya Kamati ya Utendaji ikiambatana na notisi hiyo, kivuli cha mahesabu ya Jumuiya pamoja na taarifa ya Mkaguzi wa mahesabu, na orodha ya watu walioteuliwa au wanaotakiwa kuletwa mbele ya Mkutano chini ya sheria ndogo 5.2 hapo juu.

5.5. Kwenye Mkutano wowote wa Mwaka au wa dharura wa Jumuiya, wajumbe watano au 25% ya wajumbe bila kujali uchache wao ukitoa mjumbe yoyote wa Kamati ya Utendaji watafanya akidi kwa ajili ya kuamua mambo kwenye mkutano huo.

5.6. Ikitokea ndani ya dakika theledhini (30) ya muda uliopangwa kwa ajili ya Mkutano, akidi haikutimia, Mwenyekiti ataahirisha Mkutano na kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya Mkutano huo ambao sasa hautahitaji akidi.

5.7. Baada ya Mkutano Mkuu wa Mwaka, au Mkutano Mkuu wa Dharura wa Jumuiya, Katibu atatuma nakala za kumbu kumbu za Mkutano kwa wanachama wote wa Jumuiya.

5.8. Maswala yote mbele ya Mkutano Mkuu wa Mwaka au Mkutano Mkuu wa Dharura yataamuliwa kwa kuzingatia kura za wingi wa kawaida. Wanachama wapya hawaruhusiwi kupiga kura kabla ya kujulikana na kukubaliwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka.

5.9. Bila kuathiri na kwa kuzingatia vifungu vingine vya katiba hii, theluthi mbili ya kura italazimika kwa ajili ya kupitisha maamuzi juu ya mambo yafuatayo:-
- (i) Marekebisho ya Katiba
- (ii) Kuridhia na kurekebisha sheria ndogo
- (iii) Kumuondoa/ Kumfuta kazi Mkaguzi wa mahesabu kwa namna ambayo si ya kustaafu kwa kawaida.

5.10. Kwenye Mkutano Mkuu wowote wa Mwaka au Mkutano Mkuu wowote wa Dharura wa Jumuiya, upigaji kura utakuwa kwa njia ya kunyanyua mikono labda endapo kura ya karatasi itahitajika na angalau wajumbe 1/3 waliopo binafsi au kupitia wawakilishi.

5.11. Endapo uchaguzi kwa kura ya maandishi utahitajika kuitishwa utafanya katika namna ambayo Mwenyekiti

ataelekeza na matokeo ya uchaguzi huo yatazingatiwa kuwa azimio la Mkutano huo ambapo kura ilihitajika.

5.12. Ikitokea kura zikawiana ama katika mfumo wa kunyoosha mikono au kwa mfumo wa kura za karatasi, mwenyekiti wa mkutano ambapo ni unyooshaji wa mikono ulifanyika au ambapo kura ya karatazi ilihitajika kupigwa ataamuru marudio au mzunguko mwingine wa upigaji kura.

5.13. Kulingana na ibara ya 5.10 hapo juu kuhusu unyooshaji mikono kila mjumbe aliyepo binafsi atakuwa na kura moja na katika mfumo wa kura ya makaratasi kila mjumbe aliyepo binafsi au anayewakilishwa atakuwa na kura moja.

5.14. Kwenye kura ya makaratasi kura itapigwa na mjumbe binafisi au kupitia mwakilishi. Mfumo wa kumteuwa mwakilishi utakuwa kwa maandishi ya mkono yaliyoandikwa na mteuzi na yatazingatiwa kutoa mamlaka kudai au kujiunga nakudai kura ya makaratasi.

5.15. Mwakilishi lazima awe mwanachama wa Jumuiya.

5.16. Chombo/ mfumo uliotumiwa kumteuwa mwakilishi lazima kitumwe /utumwe kwa Katibu ili kipokelewe naye si chini ya masaa 48 kabla ya wakati wa kuitisha mkutano.

5.17. Mfumo wa kumteua mwakilishi utakuwa katika mfumo ufuataoː- ( au karibu na huu kadiri hali inavyotaka au katika muundo mwingine kama huo kadiri Kamati ya Utendaji inavyoweza kuamua au kukubali kutoka wakati mmoja hadi mwingine.

5.18 Kumbukumbu za Mkutano juu ya maazimio yote na mwendelezo wa mikutano zitarikodiwa na kila kumbu kumbu ya mkutano itasainiwa naMwenyekiti wa mkutano

husika au/ na Mwenyekiti wa mkutano ufuatao na zitakuwa ushahidi tosha juu ya mambo yaliyotajwa.

**SHERIA NDOGO NO. 6.WATUMISHI**

Kamati ya Utendaji itateuwa maafisa wa Jumuiya na watumishi wengine au mawakala kwa kadiri Kamati itakavyoona ni lazima kulingana na masharti na misingi ya makubalinao kama vile mshahara na mengineyo kadiri kamati itakavyoona inafaa na kumuondoa yoyote kati yao.

**SHERIA NDOGO NO. 7. NIDHAMU.**

7.1 Kamati ya nidhamu kama ilivyotajwa chini ya sheria ndogo 3.5 itazingatia malalamiko yoyote dhidi ya mwanachama anayetuhumiwa kwa ukosefu wa nidhamu, aliofanya ama kabla au baada ya kujiunga na Jumuiya.

7.2. Mwanachama atawajibika kuchukuliwa hatua za kinidhamu kulingana na ibara hii ikitokea yoyote kati ya hali zifuatayo:-

(a) Endapo katika kufanya shughuli zake au vinginevyo ameingia hatiani kwa kosa la ukosefu wa nidhamu.

(b) Endapo ametengeneza chakula cha mifugo au amefanya shughuli zake bila ufanisi au zikiwa na kasoro kwa kiwango au idadi au matukio ya kujiharibia sifa yeye mwenyewe au Jumuiya kwa ujumla.

(c) Endapo amegundulika na Kamati ya Nidhamu kufanya shughuli zake kinyume na ubora na ufanisi unaotegemewa.

(d) Kosa jingine lolote kadiri itakavyoamuliwa na Kamati ya Nidhamu kutoka wakati mmoja hadi mwingine.

7.3. Itakuwa wajibu wa kila mwanachama na wajibu wa kila mtu kumjulisha Katibu wa Jumuiya juu ya taarifa zozote au mambo yanayoonesha kuwa mwanachama anaweza kustahiki hatua za kinidhamu kama ilivyosemwa kabla

chini ya vifungu vya ibara hii na katika hali yoyote kama hiyo itakuwa ni wajibu wa katibu kuwasilisha mambo hayo au taarifa hizo mbele ya Kamati ya Nidhamu.

7.4. Baada ya kupokea malalamiko kama ilivyoelezwa kabla, Kamati ya Nidhamu kabla ya yote itaamua endapo kwa maoni yake malalamiko yaliyowasilishwa ni moja ya malalamiko yanayopelekea au kushirikisha maslahi ya umma na endapo katika hali zote malalamiko hayo yanastahiki kushughulikiwa.

7.5. Endapo Kamati ya Nidhamu itaona kwamba malalamiko waliyoletewa yanastahiki kushughulikiwa itamjulisha mlalamikiwa mapema kadri iwezekanavyo juu ya misingi ya malalamiko hayo na wakati na pahala yalipopangiwa kusikilizwa. Kamati ya Nidhamu itampatia fursa stahiki ya kusikilizwa na endapo atapenda kitamruhusu kuwakilishwa na wakili, mwanasheria au mwanachama wa Jumuiya.

Endapo mlalamikiwa hakuhudhuria kusikilizwa kwa malalamiko kama ilivyoelezwa kabla, na endapo Kamati ya Nidhamu imeridhika kuwa wito wa taarifa wa kusikilizwa kwa malalamiko ulitolewa ipasavyo kwa mlalamikiwa kitaendelea na kumsikiliza mlalamikaji bila ya kuwepo kwa mlalamikiwa.

7.6. Endapo Kamati ya Nidhamu itaona kwamba malalamiko yamethibitishwa kwa ukamilifu au baadhi, itatoa maamuzi juu ya hilo na katika hali hiyo itatoa moja au yote kati ya maamuzi yafuatayo ikizingatia hadhi yake mlalamikiwa na mitazamo ya Kamati juu ya misingi na ukubwa wa malalamiko na mambo mengine yoyote ambayo kamati itaona yanawiana:-

(a) Kwamba mlalamikiwa afukuzwe uanachama

(b) Kwamba asimamishwe uanachama kwa kipindi kisichozidi miezi 6 kama itakavyooneshwa na hukumu.

(c) Kwamba apewe onyo kali la maandishi

(d) Kwamba apewe adhabu ya kulipa fedha taslimu za Tanzania zisizozidi Tshs. 500,000/= zitakazolipwa ndani ya mwezi mmoja.

7.7. Ikitokea Kamati ya Nidhamu kushindwa kumuwajibisha mjumbe wa Kamati au mwanachama wa kawaida, muathirika au mtu yeyote anaweza kulipeleka shauri la malalamiko kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka.

7.8. Muathiriwa yoyote anaweza kukata rufaa kwa Mkutano Mkuu wa Mwaka alimradi anafikisha taarifa ya nia yake ya kukata rufaa kwa Kamati ya Utendaji ndani ya siku 30 za kupokea barua ya kuwajibishwa na katika hali yoyote kabla ya AGM (Mkutamo Mkuu wa Mwaka, bila kuathiri sheria ndogo 5.2 hapo juu alimradi anamkabidhi Katibu rufaa yake masaa 48 kabla ya Mkutano Mkuu wa Mwaka na kulipa malipo ya fedha taslimu iliyodaiwa.

7.9. Mkutano Mkuu wa Mwaka utajadili rufaa hiyo na kutolea maamuzi na endapo maamuzi ya Mkutano Mkuu wa mwaka yatamfaidisha mlalamikaji, maamuzi ya Kamati ya Nidhamu yatabatilishwa.

**SHERIA NDOGO NO. 8. MAHESABU NA UKAGUZI WA MAHESABU.**

8.1. Mweka hazina chini ya maelekezo ya Kamati ya Utendaji atahakikisha kuwekwa kwa vitabu sahihi, vya mahesabu.

8.2. Vitabu sahihi vya mahesabu itamaanisha vitabu au kumbu kumbu muhimu ili kuwasilisha kwa usahihi hali ya mambo ya Jumuiya na kuelezea shughuli na mapato yake ya kibiashara.

8.3. Vitabu vya mahesabu vitahifadhiwa kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Jumuiya au sehemu nyingine kama itakavyoamuliwa na Kamati ya Utendaji.

8.4. Ndani ya miezi mitatu baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha wa Jumuiya, ukaguzi wa mahesabu wa mapato na matumizi, mizania, maelezo ya mtiririko wa fedha na maelezo mengine yoyote kama yatakavyoamuliwa na Kamati ya Utendaji kutoka wakati mmoja hadi mwingine ya Jumuiya utafanywa na Mkaguzi wa mahesabu.

8.5. Mkutano Mkuu wa Mwaka utateuwa Mkaguzi wa mahesabu ambaye ni mjumbe wa NBAA (Bodi ya ukaguzi wa mahesabu ya Taifa) atakayeshika madaraka mpaka mwisho wa Mkutano Mkuu wa Mwaka unaofata.

8.6. Mkaguzi wa mahesabu mteuliwa kulingana na ibara ya 8.5 hapo juu ataweza kuteuliwa kwa mara nyingine kushikilia madaraka.

8.7. Mjumbe wa Kamati ya Utendaji hatateuliwa kuwa Mkaguzi wa mahesabu kwa madhumuni ya kifungu hichi.

8.8. Mkaguzi wa mahesabu mara baada ya kuteuliwa hataweza kuondolewa isipokuwa kwa kustaafu kwa kawaida au kwa kutekeleza kifungu cha ibara ya 5.9 (iii) cha katiba hii.

8.9. Mshahara wa Mkaguzi wa mahesabu utapangwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mwaka.

**SHERIA NDOGO NO. 9. ADA**
Kutakuwa na kiingilio cha kuwa mwanachama

9.1. Kiingilio cha uwanachama kitakuwa shilingi za Kitanzania 150,000/= zitakazolipwa mara tu baada ya ombi kuwa limekubaliwa na Kamati ya Utendaji.

9.2. Ada ya michango ya mwaka itakuwa shilingi za Kitanzania 400,000/= zitakazolipwa kwa mkupuo mmoja au robo robo sambamba na ada ya uwanachama . Michango ya mwaka italipwa bila kujali tarehe ya kujiunga kama mwanachama.

Jumuiya ya Watengenezaji wa Chakula cha Mifugo Tanzania.
S.L.P. 4087,
Dar es Salaam.